# K.P.S.E.A
# TATHMINI YA SHULE YA MSINGI
# TATHMINI YA MWISHO WA MUHULA WA 2, 2026
# GREDI YA 6 -

## KISWAHILI KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA
## Muda: 20 KILA MWANAFUNZI

**TAARIFA ZA MWANAFUNZI**

Jina: ____________________________________________ Shule: ________________________________

Nambari ya Tathmini: ____________________________________ Tarehe: ________________________________

Nambari ya Shule: ______________________________________ Sahihi: ________________________________

**MAAGIZO YA JUMLA**

i. Unda mazingira rafiki ili mwanafunzi asihisi shinikizo.
ii. Mwanafunzi akae akikutazama (mmoja baada ya mwingine).
iii. Tumia mwongozo wa kutathmini kurekodi kiwango cha ufanisi.

**JEDWALI LA ALAMA**

| SEHEMU | INSHA | LUGHA | KUSI/KUZU | ASILIMIA (%) | KUZ 1 | KUZ 2 | KUF 1 | KUF 2 | KUK 1 | KUK 2 | CHI 1 | CHI12 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| KIWANGO CHA ALAMA | ALAMA 20 | ALAMA 30 | ALAMA 30 | | 90-100 | 75-89 | 58-74 | 41-57 | 31-40 | 21-30 | 11-20 | 1-10 |
| POINTI | | | | | 8 POINTI | 7 POINTI | 6 POINTI | 5 POINTI | 4 POINTI | 3 POINTI | 2 POINTI | 1 POINTI |
| JUMLA YA ALAMA ZA MWANAFUNZI | | | | | | | | | | | | |

**Sehemu A** inatathmini Stadi za Kusikiliza na Kuzungumza kupitia:

1. **Mazungumzo ya ana kwa ana**
2. **Ufahamu wa Kusikiliza**
3. **Kusoma kwa sauti**

**ZOEZI 1A: MAZUNGUMZO YA ANA KWA ANA**

**Maelekezo:**

- Mkaribishe mwanafunzi na umsalimie.
- Jitambulishe: **"Mimi ni mwalimu [Jina Lako]."**
- Anza kwa kusema: **"Leo tutazungumza kuhusu Utunzaji wa Mazingira."**

**Maswali:**

1. Mazingira safi yanapendeza na kutuepusha na magonjwa. **Je, wewe hufanya nini ili kuweka darasa lenu safi?**

   *(Mwanafunzi ajibu)*

2. Tunaweza kupanda miti na maua ili kuboresha mazingira yetu. **Taja faida mbili za kupanda miti shuleni kwenu.**

   *(Mwanafunzi ajibu)*

3. Ukimuona mwanafunzi mwenzako akitupa karatasi au plastiki kwenye uwanja wa michezo, **utampa ushauri gani?**

   *(Mwanafunzi ajibu)*

4. Tunapoyatumia maganda ya matunda kutengeneza mbolea, tunasema tunahifadhi mazingira. **Neno "kuhifadhi" lina maana gani nyingine?**

   *(Mwanafunzi ajibu)*

**ZOEZI 1B: UFAHAMU WA KUSIKILIZA**

**Maelekezo:**

- Msomee mwanafunzi kifungu hiki **mara mbili**.
- Mjulishe kuwa atajibu maswali manne baada ya kusikiliza.

**Kifungu:**

Siku ya Jumamosi, Juma na rafiki yake Musa waliamua kwenda msituni karibu na kijiji chao. Walitaka kuokota kuni na kuona ndege wa rangi mbalimbali. Walipokuwa wakitembea, waliona kuwa baadhi ya watu walikuwa wamekata miti mingi bila kupanda mingine.

Juma alihisi huzuni sana kuona msitu ukiharibiwa. Aliwaambia wanakijiji kuwa miti ni vyanzo vya mvua na makao ya wanyama. Jioni hiyo, walirudi nyumbani na kumweleza chifu wa kijiji kuhusu uharibifu huo. Chifu aliwashukuru vijana hao kwa uzalendo wao na kuahidi kuchukua hatua dhidi ya waharibifu wa mazingira.

**Maswali:**

1. Juma alienda msituni na nani siku ya Jumamosi?

   *(Mwanafunzi ajibu)*

2. Taja sababu mbili zilizomfanya Juma ahisi huzuni alipokuwa msituni.

   *(Mwanafunzi ajibu)*

3. Kwa nini chifu wa kijiji aliwashukuru Juma na Musa?

   *(Mwanafunzi ajibu)*

4. Kifungu kinasema Chifu aliwapongeza kwa **uzalendo**. Neno hili lina maana gani?

   *(Mwanafunzi ajibu)*

**ZOEZI 2: KUSOMA KWA SAUTI**

**Maelekezo:**

- Mpe mwanafunzi "Nakala ya Mwanafunzi."
- Mwambie: **"Soma kifungu hiki kwa sauti na kwa ufasaha."**
- Rekodi idadi ya maneno anayosoma kwa dakika moja na uweke alama (/).

**Kifungu cha Kusoma:**

Matumizi ya vifaa vya kiteknolojia kama vile tarakilishi na simu za rununu yameleta mabadiliko makubwa katika elimu yetu. Gredi ya sita tunajifunza jinsi ya kutafiti habari mbalimbali kupitia mtandao ili kukuza maarifa yetu. Hali hii inatufanya kuwa wabunifu na wenye uwezo wa kutatua matatizo.

Hata hivyo, ni lazima tuwe waangalifu tunapotumia vifaa hivi. Ni muhimu kulinda siri zetu na kutoingia kwenye tovuti ambazo hazitufai. Walimu na wazazi wetu hutuelekeza jinsi ya kutumia muda wetu vizuri ili teknolojia isiathiri masomo yetu mengine au afya yetu.

Ushirikiano kati ya wanafunzi unapotumia teknolojia darasani husaidia kuelewa mada ngumu kwa urahisi. Tunapaswa kuthamini vifaa hivi na kuvitunza vyema ili vitumiwe na wanafunzi wengine watakaokuja baada yetu. Maendeleo ya nchi yetu yanategemea vijana ambao wamebobea katika sayansi na teknolojia.

**MWONGOZO WA KUTATHMINI**

| **Kiwango** | **Mazungumzo (ZOEZI 1)** | **Ufahamu (ZOEZI 2)** | **Kusoma (ZOEZI 3)** |
|---|---|---|---|
| **Mbali Zaidi (4)** | Anazungumza kwa ufasaha, msamiati mpana na kujiamini. | Anajibu maswali yote kwa usahihi na maelezo kamili. | Anasoma maneno 90+ kwa dakika, anazingatia vituo. |
| **Kufikia (3)** | Anajieleza vyema na kueleweka. | Anajibu maswali mengi kwa usahihi. | Anasoma maneno 60-89, makosa ni machache. |
| **Kukaribia (2)** | Anajibu kwa kifupi au kwa kusita. | Anajibu swali 1 au 2 pekee. | Anasoma maneno 30-59, anajikwaza mara kwa mara. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Chini ya (1)** | Anashindwa kujieleza hata kwa kusaidiwa. | Hashiki maelezo yoyote ya kifungu. | Anasoma chini ya maneno 30, matamshi ni magumu. |

**HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA**